

Njia 5 za kujikinga unapo kodisha nyumba

Inawezekana huna matatizo yoyote na mwenyenyumba kwa sasa hivi. Lakini mambo yanaweza kubadilika saa yoyote kwa hiyo inakubidi ujitaarishe yakitokea matatizo yoyote. Weka vizurii na hifadhi vizuri makaratasi ya hati na risiti zote katika faili aw bahasha kubwa, alafu fanya yafwatayo.

1. Pokea risiti

Unaweza kuomba risiti, lakini sheria haimlazimisha mwenyenyumba kutoa risiti ikiwa anapokea kodi cash tu. Ikiwa mwenyenyumba hataki kufata sheria na akakataa kukupa risiti inakubidi utafute njia nyigine inayo onyesha kwamba kweli umelipa kodi. Kwa hiyo ni vizuri sana inapo wezekana kulipa kodi kwa cheki aw barua ya benki ya kumlipa mwenyenyumba kodi yake. Na uwe una shahidi wakati unapolipa kodi.

2. Andika kila kitu

Anda kila linalotokea ili uwe unaushahidi. Hakiba likitokea jambo lolote kuthibitisha msimamo wako. Andika kwa urefu majina, tarehe, na simulia yaliyotokea, na pia taarifa yoyote ilio kwa muhim.

Ikiwa unahaja ya kumueleza mwenyenyumba atengeneze kitu katika nyumba ama unataka kuhama, andika kila kitu alafu weka kopi ya barua akiba ilie kuwa imeandikwa tarehe na saina yako ju yake.

Na pia soma kwa makini kila barua ama karatasi yoyote anae kupa mwenyenyumba, kama mkataba wa kupangisha nyumba, repoti ya ukaguzi na hali ya nyumba, na barua ya taarifa yoyote.

3. Kuwa na mashahidi

Mara nyinji hutokea kuwa huna hati aw maandikiano yoyote ama huna picha. Kuwa na mashahidi ni ithibati muhimu kwa lolote linalo tokea, kama watu walio ona ama walio sikia. Shahidi lazima awe mtu alie kuwa haaishi na wewe nyumbani. Mtu unae ishi nae, mke aw mume hawawezikani kwa mashahidi wenye nguvu na wala hakubaliwi kuwa shahidi wako.

4. Chukwa picha

Saa zingie picha moja tu husema maneno elfu. Picha ni kithibitisho muhim sana. Lazima uandike tarehe na saa nyuma ya picha uliopiga. Shahidi anaweza kutia saina kuthibitisha kwamba yote yalie toka ni ukweli.

Piga picha saa hiyo hiyo inapotokea shida yoyote, kwasababu mwenyenyumba anaweza kuja na kufunika ama kubadilisha jambo lolote ukakosa dalili muhim sana.

5. Inakubidi ujuwe haki zako na wajibu wako

Linaloonekana ni jambo lakawaida si lazima jambo hilo linaweza kutendekana mbele ya sheria. Jaribu kutafuta rai ya sheria inasemaje kabla hujafanya jambo lolote ili mambo yasiwe makuba baadae.



Mtandawili (lugha tafauti): www.tenants.bc.ca
Sim ya maelezo (kizungu tu) eneo la Vancouver: 604 255-0546
Sim ya maelezo (kizungu tu) ya bure: 1-800-665-1185



**Immigrant
PLEI
Consortium**

**This project is made possible through funding from the
Government of Canada and the Province of British Columbia**